**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**

**SHULE YA SEKONDARI INGWE**
**S. L.P. 136,**
**TARIME,**
**13/05/2026**

**Email: ingwess@tarimedc.go.tz**

**Mkuu wa shule: 0763 137 359**

**Makamu mkuu wa shule: 00757 665 076**

**Mhasibu/Patron:0768207907**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………..............**

**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI INGWE, HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA, MWAKA……………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya **HGL/ HGK, HGLi, HGFa**

Shule ya Sekondari Ingwe ipo katika kijiji cha Kewanjakata ya Kemambo, Halmashauri ya wilaya ya Tarime mkoani Mara, umbali wa Kilometa 42 Kaskazini Mashariki mwa Mji wa Tarime. Kasikazini mashariki mwa mji mdogo wa Nyamongo karibu na mgodi wa North Mara Barrick Gold mine.

Wanafunzi wanaotoka nje ya wilaya ya Tarime wanapaswa kusafiri kwa usafiri wa basi hadi Tarime mjini ambapo utapata Bajaji hadi stendi ya REBU yanapopatikana magari madogo yajulikanayo kama SUCCUSED yanayosafirisha abiria hadi hapa shuleni kumbuka kuwaambia unaenda INGWE SEKONDARI utashushwa getini. Kutoka Tarime mpaka Nyamongo ni shilingi 6,000 tu.

Kwa wale wanaotokea nje ya mkoa wa Mara wanaofikia Mwanza wanapaswa kupanda basi katika kituo cha mabasi cha NYAMHONGOLO yapo mabasi maarufu ya ZAKARIA , BATCO ,KISIRE, GEORGE TOWN ambayo hufika hadi Tarime mjini.Mabasi ya kampuni ya KISIRE yapo mawili yanayofika hadi hapa Nyamongo.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………..

**Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni SKETI MBILI, moja rangi ya idara ya maji na nyingine rangi ya chokoleti inayoshonwa rinda box mbele na nyuma.Pia huku zinapatikana kwa shilingi Ishirini na Tano tu [25,000] kwa atakayehitaji.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo ni BUKTA NA TISHETI rangi ya blue ADIDAS PAMOJA NA truck suti rangi ya bluu
v. Shamba dress mbili rangi ya bluu na nyeupe viboma vidogo vidogo.(solo ndefu hadi kwenye kisigino) kitambaa gredi one. (kunguru ya bluu na nyeupe) Huku zinapatikana kwa shilingi Elfu Ishirini tu [20,000] kwa anayehitaji
vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vii. Raba za michezo pair. viii. Sokis nyeupe ndefu [[stocking].
viii. Sweta rangi ya kijani zinapatikana shuleni kwa shilingi Kumi na Mbili Elfu tu[12,000]] kwa anayehitaji

ix. Tisheti rangi ya bluu bahari inapatikana shuleni kwa shilingi Kumi na Mbili Elfu tu(12,000) kwa anayehitaji

x. Track suit moja ya Bluu inapatikana shuleni kwa shilingi Ishirini Elfu tu [20,000/=] kwa anayehitaji

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counterbook QUIRE 3 (7) pamoja na madogo ya msomi (4)

ii. **Ream paper (double A)** BANDO (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Godoro fut 2.5/6

v. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki na bluu , blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1

vi. Nguo za ndani za kutosha; pamoja taulo za kike za kutosha, n na Kanga

vii. Box files 2 (ALBALADA)

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko; moja kwa ajili ya matumizi ya shule.

x. Tahasusi ya HGL aje na Kwanja 1, squizer 1 fagio 1 wa ndani

xi. Tahasusi ya HGK aje na Jembe 1, reki 1, fagio 1 wa nje

xii. Dumu cha LTR 5 cha kutunzia maji ya kunywa.

xiii. Dawa ya choo 10 LTR

xiv. Dawa ya mbu (HIT 750MLS) 2

xv. Tranka la bati na kufuri kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake

xvi. Fedha za matumizi binafsi (zitunzwe kwa MHASIBU wa shule ili kuepuka wizi bweni.)

xvii. **AJE NA BIMA YA AFYA (NI MUHIMU)**

**Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB. Malipo yafanyike katika akaunti ya shule yenye jina INGWE SECONDARY SCHOOL Ac/No. 30401200146 NMB na mwanafunzi awasilishe PAY INSLIP kwa Mhasibu wa shule mara atakaporipoti shuleni.**

**Aidha mwanafunzi asiye na kadi ya bima ya afya anatakiwa kwenda Tshs 50,400 taslimu.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bilataarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

5. v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba; xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. **KARIBU SANA**

**....................**

**ELIKA M. SIMU**

**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.**













**INGWE SEKONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION**

Full name ..........................................................................................................................................

Age ..................... Height (in cms) ...................... weight (in kgs)..............................................

1. Blood count ................................. (red and white ) ...........................................................

2. Stool examination ..........................................................................................................

3. Urine analysis ................................................................................................................

4. Syphils and other V.D ....................................................................................................

5. T.B and Leprosy test ......................................................................................................

6. Eye test ..........................................................................................................................

7. Ear test ..........................................................................................................................

8. Chest test .......................................................................................................................

9. Abdominal test ..............................................................................................................

10. Blood group (very crucial ) ..........................................................................................

11. Spleen .............................................................................................................................

12. HIV test , postive ............ negative ............( tick where necesary )

Adiditional information e.g physical defect or imperements , infections , chronic or family desease ( eg. Sickle cell)

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

I ceticify that the above student is fit/is not fit to pursue secondary education

Signature ……………………………………

Designation …………………………………

Station ……………………………………………

Date ………………………………………………

***This form must be returned on reporting day***

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI INGWE**

**<u>HISTORIA / TAARIFA YA MWANAFUNZI.</u>**

1. Jina la ukoo ........................... Jina la kwanza .......................... Jina la kati ...........................
2. Jina la mzazi / mlezi ..................................................namba ya simu ...................................
3. Kama ni mlezi uhusiano ................... namba ya simu.............................................................
4. Anwani ya kudumu ya mzazi ama mlezi .................................................................................
5. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi ...........................................................................................
6. Mahali mwanafunzi alipo zaliwa: Kijiji cha ..............................Kata ya ...........................
   Wilaya ....................................... Mkoa wa .........................................
7. Dini ........................................... dhehebu ..............................................................................
8. Unaingia kidato cha .......................................tarehe /mwaka .............................................
9. Kutoka shule ya sekondari .............................wilaya .......................... Mkoa............................
10. Mzazi / mlezi anafanya kazi ajira /mkulima / biashara ..................................................
11. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari / taarifa muhimu juu yako

I. ........................................uhusiano ........................... namba ya simu ............................

II. .........................................uhusiano .......................... namba ya simu............................

III. ...........................................uhusiano ...........................namba ya simu..........................

12. Sifa maalumu kama unazo...................................................................................................
13. Taarifa za wazazi. Wapo wote ...................................... ii. Yuko mmoja (taja BABA / MAMA ................................................ iii. WOTE WAMEFARIKI ............................ ,(weka alama vema panapo husika )

Nakiri kuwa maelezo yaliyopo hapo juu ni sahihi.

..................................... ..............................

SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI / MLEZI

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi (jina la mwanafunzi)........................................................ nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga shule hii. Naahidi kufata sheria za shule na taratibu zote zilivyotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

**AHADI YA MZAZI / MLEZI**

Mimi (jina) ........................................................... ambaye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi ..............................................nimeyasoma mashariti na sheria za shule ya sekondari Ingwe ambako binti wangu amechaguliwa kujiunga. Naahindi kuwa nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia mwema wa Taifa letu.

Tarehe ..................................

Jina la mwanafunzi ....................

Sahihi ya mwanafunzi ......................

Tarehe ............................................

Jina la mzazi / mlezi ..................................

Sahihi ya mzazi / mlezi .........................